1) Mtahiniwa afafanue jinsi fasihi andishi ilivyofuata nyayo za fasihi simulizi katika uundwaji wake kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo:
   (a) Ujenzi wa Muundo
   (b) Ujenzi wa Mtindo
   (c) Ujenzi wa Wahusika
   (d) Matumizi ya lugha
   (e) Ujenzi wa Mandhari
   (f) Dhamira zinazoelezwa
   **Mgawanyo wa alama**
   ***Utangulizi – 01***
   ***Hoja 6@1.5 = 09***
   ***Jumla = Alama 10***

2) Mtahiniwa afafanue dhana zifuatazo;
   (a) Utao – Ni kipande cha pili cha mshororo katika ubeti wa shairi.
   Mfano;
   Kinda ningali mtini, sina mama kunilea
   ↑
   Utao

   (b) Mizungu – Ni kauli zenye mafumbo zinazoonesha ukinzani wa fikra au tukio hasa katika semi. Mfano; Papai limeiva nyumbani, ila siwezi kulila.
   (c) Tarihi – Ni hadithi zinazohusu matukio muhimu ya kihistoria. Mfano; Matukio yote ya kihistoria yaliyo ya kweli na kubuni.
   (d) Maghani – Ni tungo za Ushairi zinazotongolewa kwa kutumia sauti iliyo kati ya uimbaji na uzungumzaji.
   Mfano; Mwanamziki Mrisho Mpoto hutumia maghani katika uwasilishaji wa fani yake.
   (e) Lakabu – Ni majina ya kupanga ambayo baadhi ya watu hupewa au hujipa kutokana na sifa zao za kimaumbile, kinasaba, kitabia, kiujuzi au kimatendo.
   Mfano; Mwamba – Mtu Imara, mwenye nguvu, jembe – mchapakazi
   - **Mtahiniwa anaweza kutoa mifano mingine, apewe alama kama ni sahihi**
   ***Alama***
   ***1@2 × 5 = 10***

3) Mtahiniwa aeleze faida udhamini katika kazi za fasihi. Hoja zifafanuliwe kwa ufupi na mifano halisi.
   (i) Husaidia baadhi ya wasanii kufanya tafiti za masuala mbalimbali yanayohusu jamii. Mfano waigizaji wa sanaa mbalimbali zikiwemo maigizo yanayoonesha Maisha halisi ya jamii.
   (ii) Husaidia jamii kupata kazi mbalimbali za fasihi, hasa fasihi andishi mfano; vitabu mbalimbali vya fasihi vya kiada na ziada.
   (iii) Husaidia kuibua na kuendeleza vipaji hasa vya wasanii chipukizi ambao Uchumi wao si imara. Mfano; waandishi wachanga, waigizaji wachanga, wanamziki wanaoanza.
   (iv) Husaidia wasanii kujipatia kipato hasa pale kazi zao zinapouzika sokoni. Mfano; Wasanii wote wadogo na wakubwa kwa fani zote.
   (v) Husaidia kuleta ushindani wa ubora wa kazi mbalimbali za fasihi katika soko la kazi za fasihi.
   (vi) Husaidia mwandishi na mdhamini kujulikana kutokana na kazi zinazotolewa. Mfano; Waandishi wanaodhaminiwa na Taasisi ya Elimu Tanzania hufahamika kupitia TET.
   - **Mtahiniwa anaweza kuandika hoja nyingine ambazo ni sahihi apatiwe alama.**
   ***Alama***
   ***1@2 ×5 = Alama 10***

4) Mtahiniwa anatakiwa kuonesha mbinu za kifani zilizounda Makala aliyoisoma. Mbinu hizo ni kama hizi zifuatazo.

(a) Muundo; Ni mbinu ya Kisanaa ya Utungaji wa kazi ya fasihi inayofuata mpangilio maalumu wa visa na matukio. Katika utanzu wa Ushairi Muundo huangaliwa kwa idadi ya mistari katika ubeti, katika shairi hili Muundo wake ni sabilia kwa sababu shairi limeundwa na mistari mitano (5) kwa kila ubeti.

(b) Mtindo; Ni jinsi au namna mwandishi wa kazi ya fasihi alivyojenga kazi yake.
Katika shairi hili mwandishi ametumia mtindo wa kisasa usiofuata kanuni za mfanano wa vina na mizani katika mstari mmoja; kwani shairi hili lina mistari mitano kwa kila ubeti, vina vyake havifanani na mizani hazifanani.

(c) Matumizi ya lugha; Ni namna mtunzi au msanii alivyotumia lugha katika kazi yake ya fasihi.
Katika shairi hili mwandishi ametumia Tashibiha (Itikadi ya mapinduzi ni sukari.)

(d) Wahusika; Ni viumbe hai na visivyo hai ambao mwandishi huwatumia kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa hadhira anayoiandikia. Katika shairi hili wahusika ni wale wote wanaokandamizwa na kuonewa katika jamii wanaotaka kujikomboa ili kuondokana na ukandamizwaji wa unyonywaji.

(e) Mandhari; Ni mahali popote pale ambapo kazi ya fasihi inatendeka/ kufanyika. Katika shairi hili mandhari ni mahali popote ambapo ukandamizaji na unyonyaji unaendelea. Kwa maneno mengine mandhari si halisi au si sehemu fulani maalum.

***Alama 1@2 × 5 = 10***

5) Mtahiniwa afafanue taswira mbalimbali zilizopo katika vitabu vya ushairi alivyosoma kama ifuatavyo:

FUNGATE YA UHURU (TASWIRA)

(i) Fungate – Sherehe
(ii) Waja wa Mungu – wanaonyanyasika, wakandanizwao
(iii) Utawala – Uongozi
(iv) Unganeni – Ushirikiano
(v) Gorila – Mapinduzi

KIMBUNGA (TASWIRA)

(i) Wazazi – Kuhimiza malezi/ uwajibikaji katika malezi
(ii) Si vyema – Nidhamu/Utu
(iii) Wacha haya – Kuacha umbea
(iv) Punda – Kutoa shukrani
(v) Dawa ya deni kulipa – Umuhimu wa kulipa deni

MAPENZI BORA (TASWIRA)

(i) Pambo la moyo
(ii) Pumuuzi
(iii) Urafiki wa wawili } Mapenzi
(iv) Chanzo cha fujo
(v) Mshipa wa damu

CHUNGU TAMU (TASWIRA)

(i) Chungu Tamu – Mategemeo
(ii) Chatu na Kuku – Dhuluma
(iii) Chini ya mti mkavu – Dhuluma
(iv) Daktari Askari – Uwajibikaji (kazi)
(v) Wimbo wake hotubani – Uongozi mbaya

**Mtahiniwa anaweza kutoa taswira tofauti na hizi lakini ziendane na kila kitabu apatiwe stahiki zake.**

***Utangulizi – 01***
***3@1=3 × 6 = 18***
***Hitimisho – 01***
***Jumla = 20***

6) Mtahiniwa ajadili dhamira zilizojadiliwa na waandishi wa vitabu vya ushairi alivyovisoma kama ifuatavyo:

CHUNGU TAMU

(i) Kupinga dhuluma – Chatu na Kuku, chanzo ni wenye kauli, chini ya mti mkavu nk.
(ii) Kufanya kazi kwa bidii – Chanzo ni wenye kauli, wimbo wake hotubani, Daktari Askari, wengine wabaki Taabuni
(iii) Kuwa na uongozi mzuri – Tishio la binadamu, chini ya mti mkavu, wanajua kuvumilia/ udongoni.
(iv) Kuwepo na demokrasia ya kweli – kademokrasi katoweka
(v) Kupiga vita matabaka – Manzese mpaka Ostabei, Thomasi na Doto, Chatu na Kuku, wimbo wake hotubani.
(vi) Kuepuka vita – Tishio la binadamu, Daktari Askari.
(vii) Mapenzi – Daktari Askari; Ngulu wapaona, Thomasi na Doto, Takumbuka Daima, Usiwe mwonja Asali, Fikra za waungwana
(viii) Nafasi ya mwanamke – Daktari Askari, Manzese mpaka Ostabei, Fikra za Waungwana.
(ix) Wosia – Wosia

MAPENZI BORA

(i) Maana ya Mapenzi Bora
(ii) Sifa za Mapenzi Bora
(iii) Faida za kuwepo kwa mapenzi bora katika jamii
(iv) Hasara za kukosekana kwa mapenzi bora katika jamii.

KIMBUNGA

(i) Umuhimu wa malezi Bora – Vijana wa Zanzibari
(ii) Uongozi mzuri – Kimbunga, siyu, madanganyo wenye vyao watubana, kimbwangai.
(iii) Kupiga vita rushwa – Rushwa
(iv) Umuhimu wa elimu – kisomo cha manufaa
(v) Kupiga vita ukoloni mamboleo – chuwi
(vi) Umuhimu wa kujitawala – Afrika, kujitawala
(vii) Umuhimu wa kazi na kuwajibika – kazi mkarafuu, Dumuzi
(viii) Mapenzi na ndoa – Usimpige mkeo, Hongera, sifa ya mke, sitaki
(ix) Maradhi ya hatari – vielelezo, usafi, mnapata kitu gani.

FUNGATE YA UHURU

(i) Kuwa na uongozi bora – Fungate, waja wa Mungu, wizi, viongozi wa Afrika, utawala, njama, kinyang'anyiro, ujamaa
(ii) Kuwa na umoja na ushirikiano – unganeni, Nikizipata Bunduki
(iii) Ujasiri na kujitoa mhanga – Gorila, umma
(iv) Kufanya mapinduzi (mageuzi)- Umma, Unganeni, siku itafika, Nikizipata Bunduki, utawala, mjamzito, maendeleo ya umma, Ni vita si lelemama.
(v) Kuwa na uzalendo katika nchi – Nchi yangu.
(vi) Kupiga vita ukoloni mamboleo – Ruya, Kunguru.
(vii) Kupiga vita wizi wa mali ya umma, wizi, kunguru, Naona, Joka la Mdimu.
(viii) Kupiga vita ukasuku wa viongozi wetu Afrika.
(ix) Mapenzi – Nchi yangu, Nia yangu sigeuzi, uwapi uzuri wako, Kantu sauti ya kiza, wewe peke yako, Ua si ruwaza njema.

***Utangulizi – 01***
***3@1=3 × 6 = 18***
***Hitimisho – 01***
***Jumla = 20***

7) Mtahiniwa ajadili Dhamira zilizopo katika vitabu viwili vya Tamthiliya alivyovisoma.

NGUZO MAMA

(i) Uongozi mbaya – mfano Mwenyekiti

(ii) Dhuluma – mfano – Bi saba

(iii) Elimu – mfano – wanawake wa Patata, Bi nane

(iv) Usaliti – Waalimu

(v) Umaskini na Magonjwa – mfano, Bi tano, chizi

(vi) Uvivu na uzembe – Bi moja, Bi tano, Bi sita

(vii) Mapenzi na ndoa – mfano; Bi sita, Bi tatu

(viii) Nafasi ya mwanamke – Bi sita,

KIVULI KINAISHI

(i) Umuhimu wa uongozi bora

(ii) Kufanya mapinduzi

(iii) Kujitoa muhanga

(iv) Nafasi ya wakati

(v) Demokrasia ya kweli

(vi) Umuhimu wa Elimu

(vii) Kupiga vita Rushwa

(viii) Kupiga vita matabaka

(ix) Nafasi ya mwanamke
(x) Ushirikina/ uchawi
(xi) Hali ngumu ya Maisha (umaskini)

MORANI
(i) Kupiga vita uhujumu Uchumi
(ii) Kupiga vita unafiki na usaliti
(iii) Kupiga vita matabaka
(iv) Kujitoa mhanga
(v) Kuwa na umoja na mshikamano
(vi) Nafasi ya mwaname katika jamii
(vii) Mapenzi

KWENYE UKINGO WA THIM
(i) Nafasi ya mwanamke katika jamii
(ii) Malezi
(iii) Ndoa
(iv) Dhana potofu
(v) Utekelezaji mbaya wa mipango ya maendeleo ya Taifa

**Mgawanyo wa alama**
**Utangulizi – 01**
***3@1=3 × 6 = 18***
***Hitimisho = 01***
***Jumla = 20***

8) Mtahiniwa ajadili dhamira za vitabu viwili vya Riwaya alivyovisoma.

MFADHILI

(i) Usaliti
(ii) Umuhimu wa uongozi mzuri
(iii) Bidii katika kazi
(iv) Chuki
(v) Dharau
(vi) Nafasi ya Mwanamke
(vii) Usaliti

VUTA N'KUVUTE

(i) Ukombozi
(ii) Mapenzi na ndoa
(iii) Mivutano baina ya wazazi
(iv) Matabaka
(v) Nafasi ya mwanamke katika jamii
(vi) Dhana potofu na dharau
(vii) Uvumilivu na ujasiri katika Maisha
(viii) Umoja na mshikamano
(ix) Usaliti

KUFIKIRIKA

(i) Uongozi
(ii) Ugumba na Utasa
(iii) Bidii katika kazi
(iv) Matibabu kwa mitishamba
(v) Majivuno na dharau
(vi) Umuhimu wa elimu
(vii) Nafasi ya mwanamke katika jamii
(viii) Shukrani

USIKU UTAKAPOKWISHA

(i) Suala la uongozi na rushwa
(ii) Hali ngumu ya Maisha
(iii) Mapenzi
(iv) Tatizo la usafiri
(v) Nafasi ya mwanamke

**Mgawanyo wa alama**
**Utangulizi – 01**
***3@1= 6× 3 = 18***
***Hitimisho = 01***